

TALKING NOTES ZA KATIBU MKUU KIONGOZI KATIKA BONANZA LA SHIMIWI TAREHE 20 AGOSTI, 2022 UWANJA WA JAMHURI, DODOMA.

Ndugu Viongozi wa SHIMIWI,
Ndugu Makatibu Wakuu mliopo,
Ndugu wanamichezo na Watumishi wa Umma mliopo,
Ndugu wanahabari,
Mabibi na Mabwana,
Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Kwanza kabisa napenda kumshukuru MUNGU kwa kutuwezesha kufika hapa kwa ajili ya

Pili, Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza watumishi wa Umma nchini kote ambao wanajitoa usiku na mchana, kutekeleza majukumu makubwa na mazito ya kuijenga nchi yetu, napenda pia kuwashukuru watumishi wa Umma wanamichezo ambao mmepata fursa ya kujumuika hapa leo kwa ajili ya kufanya mazoezi kwa Pamoja.

Tatu, Napenda kuishukuru Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Baraza la Michezo la Taifa kwa kazi nzuri mnayofanya katika kusimamia michezo nchini. Michezo ni ni furs ana ni muhimu watanzania wakaitumia kikamilifu.

Nawashukuru sana Watumishi Waandamizi wa Wizara ambao wapo hapa leo, Katibu Mkuu (TAMISEMI), Katibu Mkuu (Utamaduni, Sanaa na Michezo) na Naibu Katibu Mkuu (UTUMISHI),

Ndugu watumishi wa Umma na wanamichezo, Jukumu la msingi la watumishi wa Umma ni Pamoja na:-

- i. Kutoa huduma bora kwa Watanzania,
- ii. Kufanya kazi kwa bidii na weledi ili kuleta matokeo chanya,
- iii. Kuongeza ubunifu na tija katika shughuli za Serikali ili kuinua ubora wa huduma za Serikali,

- iv. Kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Utumishi wa Umma katika kutekeleza shughuli za kila siku.

Watumishi wa Umma ni chachu ya Maendeleo ya Taifa, ni sisi ambao tunaandaa na kupanga mipango yote na kutoa Mwelekeo/Dira ambayo nchi inafuata. Aidha, Watumishi wa Umma ndiyo wanaosimamia utekelezaji wa Mipango hiyo.

Kama sehemu ya jamii, Watumishi wa Umma lazima tuwe na uhakika wa mahitaji ya msingi ya wananchi ili kupelekea kuandaa mipango bora inayolenga kuinua Maisha ya wananchi wote na pia kusimamia utekelezaji wake ili kufikia malengo tuliyojiwekea.

Ili kutekeleza majukumu haya mazito, Watumishi wa Umma hawana budi kuwa na afya njema na akili timamu. Masuala haya unayapata katika Mtindo bora wa Maisha (Healthy Living). Mtindo bora wa Maisha ni ule unaozingatia ulazi unaofaa, kufanya mazoezi ya mwili, kuepuka matumizi ya Sigara au bidhaa za Tumbaku. Utaratibu huu unasaidia kukabiliana na magonjwa sugu yasiyoambukiza kama vile Ugonjwa wa Moyo, Kisukari n.k hivyo kulinda nguvu kazi ya Taifa.

Ni kwa kutambua hili Serikali ilianzisha taasisi ya kusimamia michezo katika Wizara za Serikali ili kutoa fursa ya kujenga dhana ya mtindo bora wa Maisha. Maeneo mengine ya manufaa ni Pamoja na kujenga umoja katika Utumishi wa Umma kwa watumishi kupata nafasi ya kujenga ushirikiano (networking). Serikali ni kubwa na ina malengo tofauti ingawa malengo hayo yote, mwisho wake ni kutimiza lengo kuu la Serikali. Bila kuwa na umoja, ni vigumu kutimiza malengo hayo. (Science of Football kwenye Governance). Tutumie michezo kujenga umoja ili malengo ya taasisi zetu yaweze kutimia.

Kama mnavyojua, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepanga kufanya Sensa ya Watu na Makazi. Kwa sasa, maandalizi yamekamilika na Sensa hiyo itaanza siku ya Jumanne, tarehe 23 Agosti 2022. Sensa ya Watu na Makazi ni zoezi la kitaifa linalofanyika kila baada ya miaka 10 ambapo Sensa ya mwisho kufanyika nchini ni ile ya mwaka 2012. Hivyo Sensa ya mwaka 2022 itakuwa ni sensa ya Sita kufanyika nchini baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964. Sensa nyingine zilifanyika mwaka 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012.

Ndugu watumishi wa Umma na wanamichezo, Mwaka huu ni mwaka wa Sensa ya watu na makazi. Sensa ya watu na makazi ni utaratibu wa kukusanya, kuchambua, kutathimini na kuchapisha na kusambaza takwimu za kidemographia, kiuchumi na kijamii kuhusiana na watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalum. Kwa maana nyingine, sensa ni zoezi maalum lenye lengo la kupata idadi ya watu wote

katika nchi, kwa umri na jinsia, mahali wanapoishi na hali yao ya elimu, hali ya ajira, hali ya vizazi na vifo na hali ya makazi. Takwimu hizi za msingi ndiyo zinazoweza kuanisha mahitaji halisi ya wananchi yakiwemo makundi maalum yenye uhitaji maalum kwa mfano, watu wenye ulemavu, wanawake, watoto, vijana na wazee hivyo kurahisisha uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo kulingana na uhitaji na mazingira yaliyopo.

Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ina Umuhimu wa kipekee ambao ni pamoja na:-

1. Kuisadia Serikali kupata taarifa za msingi zitakazosaidia mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025, mageuzi ya masuala ya afya na jamii, pamoja na ufuatiliaji wa ajenda za maendeleo za kimataifa;
2. Taarifa za idadi ya watu husaidia katika mamlaka za wilaya katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo huakisi matakwa ya watu katika ngazi husika na kusaaidia kwenye uwiano wa mgawanyo wa rasilimali;
3. Taarifa za msingi za hali ya kidemografia, kijamii na kiuchumi za idadi ya watu na makazi za mipango katika ngazi zote;
4. Kigawio katika kukokotoa viashiria vingine mfano Pato la mtu mmoja mmoja, Pato la Taifa, Ajira na ukosefu wa Ajira na kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi;
5. Taarifa itakayowezesha serikali kujua ongezeko la idadi ya watu, kwa mgawanyo na viashiria vingine, ambavyo ni muhimu kwa usimamizi wa mazingira; na
6. Msingi wa utawala bora na ujumuishaji wa demokrasia. Takwimu sahihi za Sensa zinahitajika kwa ajili ya ugawaji wa majimbo ya uchaguzi kwa ufanisi, kurekebisha mipaka ya kiutawala katika serikali za mitaa.

Wakati nahitimisha, naomba kusesitiza yafuatayo:

- i. Michezo ni sehemu ya kazi hivyo, Wakuu wa Taasisi waone umuhimu wa kutenga bajeti kwa ajili ya michezo, ikiwa ni pamoja na kuwapa watumishi ruhusa za kuhudhuria michezo na mashindano mbalimbali kama ilivyobainishwa kwenye kanuni za Utumishi wa Umma,
- ii. Utendaji kazi unaojali matokeo,
- iii. Watumishi wa Umma kuongeza bidi katika kutekeleza shughuli za Umma ili kufikia malengo ambayo nchi yetu imejiwekea,
- iv. Kuwa tayari kuhesabiwa siku ya tarehe 23 Agosti, 2022.

Nawatakia kila la kheri katika zoezi la Sensa na Michezo mema ya SHIMIWI 2022 itakayofanyika Tanga kuanzia tarehe 1 - 15 Oktoba, 2022.

Asanteni sana.